MUHTASARI WA UTENDAJI NA MAPENDEKEZO



# C S W D

Chama cha maendeleo ya wanawake wa Chole **TANZANIA**

Pat Caplan na Christine Walley

Kvinnefronten /Wanawake mbele Norway

CSWD

Chama Cha Maendeleo Ya Wanawake Wa Chole
P.O. Box 33, Mafia Island, Tanzania

CSWD
Chama Cha Maendeleo Ya Wanawake Wa Chole, Mafia Island, Tanzania
Muhtasari wa Utendaji na Mapendekezo

Pat Caplan na Chrisine Walley
Boston/Chole/London, Tathmini 2004

© Kvinnefronten/Wanawake mbele Norway
Mada imepata msaada kutoka kwa Wanawake mbele Norway/FOKUS/Norad

Mtoaji: Kvinnefronten/Wanawake mbele Norway
Osterhaugsgata 27
0183 Oslo, Norway
Simu/fax: + (47) 22 20 64 00
e-mail: kvinnefronten@online.no

www.kvinnefronten.no
www.fokuskvinner.no

Matayamisho: Camilla Løland na Thera Mjaaland
Picha: Agnete Strøm

Kime tolewa na Allkopi

# CSWD

CHAMA CHA MAENDELEO YA WANAWAKE WA CHOLE
MAFIA, TANZANIA


TEXTILE

*"Na tulipotoa maelezo yetu na kuwaonyesha video na mambo tuliyoyafanya, japokuwa wao walipata pesa nyingi za msaada walikiri na kusema 'kwa kweli sisi bado hatujaweza kufanya mambo yote haya kama mliyoyafanya nyinyi'."*





# Fahirisi


**1 MUHTASARI WA UTENDAJI** 11
Utangulizi, njia na malengo 11
Mazingira 12
Miradi na mafanikio ya CSWD 12
Uongozi na uwezo 12
Maswala yaliyojitokeza 14

**2 HITIMISHO NA MAPENDEKEZO MAALUMU** 17
'Maendeleo', 'uendelevu' na 'uongezaji uwezo' 17
Uongozi 18
Meneja mradi/mshauri wa kiufundi wa CSWD 19
Kuendeleza mawasiliano, ushirikiano na uwazo 20
Mgawanyo wa faida, mgawanyo wa majukumu 23
Namna ya kukabili magomvi katika jamii 24
Kipindi cha kati na kirefu cha hali ya baadaye ya CSWD 25



# 1

# Muhtasari wa utendaji

## Utangulizi, njia na malengo

Chama cha Maendeleo ya Wanawake wa Chole (CSWD) kilianza mwaka 1997 na kilisajiliwa mwaka 2000 kimekuwa kikipokea michango ya fedha kutoka Wanawake mbele/FOKUS, Norway toka mwaka 1997, ambao pia waligharamia utathmini wa chama hiki. Utathmini huu uliendeshwa na wanaanthropologia wawili wenye uzoefu mkubwa na wa muda mrefu wa kufanya utafiti katika kisiwa cha Mafia.

- Malengo ya utathmini huu yalikuwa ni kutoa taarifa stahilifu itakayosaidia kujifunza tofauti iliyoletwa na uwepo wa CSWD. Taarifa ya utathmini huu ilikuwa hasa ni kwaajili ya hadhira ya wanachama wa CSWD, Wanawake mbele and FOKUS pamoja na vikundi vingine vya akina mama vilivyoko nchini Tanzania na mahali pengine.

- Wakati wa utafiti huko Chole, mkazo ulitiliwa kwenye kukusanya taarifa bora na ya undani kupitia mahojiano na mikutano katika vikundi, mahojiano ya mtu mmoja mmoja kwa washiriki wakuu, uangalizi wa shughuli kuu za Chole na uhakiki wa nyaraka muhimu.

- Watathmini pia walikusanya maelezo mengi ya nyuma kutoka vyanzo mbalimbali ambavyo vilikuwa muhimu katika kuiweka CSWD katika mazingira halisi ya jamii ya watu wa Chole.

- Watathmini hawa walitumia muda wa wiki mbili na nusu kufanya kazi hii juu ya Chole mwezi wa julai 2004.

- Karibia na mwisho wa kukaa kwao huko Chole, watathmini walitengeneza taarifa ya awali katika Kiswahili ambayo ilijadiliwa kwa upana katika mikutano ya wanachama wa CSWD pia na Serikali ya Kijiji.

- Watathmini pia waliweza kutoa mchango wao katika kusadia kuandika kielelezo cha awali cha kazi na maelezo maalum ya mtu kwa kazi ya Afisa Maendeleo ya Jamii hali kadhalika walitoa msaada katika kuratibu mpangilio wa kutayarisha orodha ya awali ya nafasi ya kazi.

## Mazingira

- Chole ni kisiwa kidogo chenye uchumi wa fedha na ule wa kujikimu kwa mazao ya chakula. Uchumi wake wa fedha unatokana na uuzaji wa nazi, machungwa pamoja na uvuvi. Hivi karibuni vyanzo hivi vya fedha vimekuwa vikididimia kusababisha maisha ya sasa kujulikana kama kipindi cha "maisha magumu". Tofauti kati ya wanajamii, kihali na mali imeanza kuwa dhahiri.

- Mahusiano ya kijinsia baina ya wenyeji wa Chole hayaelezeki kwa urahisi. Wanawake wana majukumu mengi zaidi ya kazi, wanamiliki vitu vichache kuliko wanaume na kufuatana na historia wanawake walikuwa na nafasi duni za kwenda shule. Hata hivyo wanawake bado wana sauti katika mambo fulani kama vile kuweza kumiliki mali bila kulazimika kuhusisha waume zao. Zaidi ya hayo, mahusiano ya kijinsia yanabadilika kutokana na kuongezeka kwa nafasi za kimasomo kwa pande zote yaani wake kwa waume, na kwa sababu kipindi hiki kinafahamika kama cha wakati mgumu basi mchango wa wanawake na wanaume wote kwa pamoja ni muhimu na unahitajika sana.

- Kwa mazingira ya kisiasa, wanakijiji wa Chole, kama ilivyo wakazi wengine wa Mafia, wanaona kwamba Wilaya yao haipewi nafasi sawa ukilinganisha na sehemu nyingine za Tanzania. Uongozi wa kijiji umeshuhudia mabadiliko makubwa hivi karibuni, kupitisha utawala kutoka kizazi kimoja kwenda kingine, hivyo uongozi wa kijiji ulijaribu vikali kuhakikisha kuwa shughuli zote zinabaki chini ya mamlaka yake, hii ikiwa ni pamoja na CSWD.

- Katika kijiji cha Chole pia kuna hoteli ya kitalii ambayo inaendeshwa na wataalamu kutoka nje. Hoteli hii ilianzishwa ikiwa ni sehemu mojawapo ya kutia moyo maendeleo ya jamii na ambayo pia huchangia fungu la fedha katika shughuli za kijamii kutokana na ushuru inayozalishwa.

- Mingi ya misaada ya chama cha CSWD inatoka katika shirikisho la Wanawake mbele/FOKUS ambalo dhumuni lake kubwa ni kuunda Mshikamano wa Kimataifa wa Wanawake.

## Miradi na mafanikio ya CSWD

- Chama cha CSWD kimepata mafanikio makubwa kwa muda wake mfupi toka kianzishwe, kimejenga na kinaendesha Kituo cha Afya, soko, Chekechea na Kituo cha Kujifunzia.

- Pia kimeanzisha vikundi vya Akiba na Mikopo, msaada wa masomo kwa wasichana waendao shule za sekondari, Madarasa ya Elimu ya Watu Wazima katika masomo mbali mbali pamoja na programu za utambuzi wa ugonjwa wa Ukimwi.

- Kwa kiasi fulani chama hiki hakikufanikiwa sana katika majaribio yake ya kuzifikia jamii jirani.

## Uongozi na uwezo

- Chama cha CSWD ni chama kilichosajiliwa chini ya sheria ya Tanzania. Kina kamati ya watu 13, wakiwemo Mwenyekiti, Katibu na Mwekahazina, ambao huchaguliwa kila baada ya miaka miwili. Pia kuna safu ya kamati ndogo ndogo zinazosimamia miradi mbali mbali.

- Wanawake wote wa Chole wanachukuliwa kama wanachama wa CSWD

- CSWD pia ina Meneja Mradi aliyesomea kazi za maendeleo na mwenye uwezo wa kutumia lugha za Kiswahili na Kiingereza kwa usanifu, ni mmoja wa watunza hoteli iliyoko kisiwani. Kazi yake imekuwa ni kusaidia na kuratibu kuandika miswada na taarifa za miradi.

- Wanachama wa CSWD hasa viongozi na wahamasishaji wamenufaika kutokana na mafunzo na uwezo wao umezidi kuongezeka katika nyanja mbalimbali ikiwa ni pamoja na utawala na uongozi. Hatahivyo kumekuwa na ukosoaji na wivu juu ya haya kutoka kwa wanawake wanachama ambao sio wahamisishaji na wanakijiji wengine.

# Maswala yaliyojitokeza

- Watu wengi wa Chole walieleza hisia zao za kutengwa kutoka katika shughuli na faida za CSWD.

- Ukosoaji ulitoka hasa kwa wakazi wa Kilimani, moja ya kijiji kidogo kati ya vijiji vya Chole, ambacho kihistoria kimekuwa kikionyesha hali ya kuonewa kiuchumi kulinganisha na sehemu nyingine.

- Swala kuu katika ukosoaji lilikuwa ukweli kuwa wengi wa viongozi wakuu wa CSWD walitoka sehemu moja ya kijiji na walikuwa ndugu wa karibu.

- Wakosoaji wa CSWD, ambao wameanzia kwenye Serikali ya Kijiji hadi wakazi wa Kilimani, walitoa hoja kuwa hawakupewa taarifa za kutosha kuhusiana na shughuli za CSWD. Ni wazi kuwa, ingawa CSWD imefanya bidii kubwa kuwaeleza watu juu ya mipango na shughuli zake, kazi hii si rahisi kufanyika katika jamii ambayo rasilimali zake ni duni

- Baadhi ya viongozi na wahamisashiji wa CSWD walitoa hoja zao kuwa wao pia wangependa kujifanyia mambo mengi wao wenyewe, kwa mfano kuandika taarifa na miswada.

- Baadhi ya maudhi dhidi ya uongozi wa CSWD yalitokana na wivu juu ya uongozi, kuwa wana njia za kupata fedha za misaada ya nje, lakini hii inatokana na kutokufahamu namna fedha za misaada zinavyofanya kazi na vikwazo kwa watumiaji wake.

- Pia kuna mgogoro kuhusiana na mkazo wa miradi ya CSWD, ambayo inawanu faisha wanawake au wasichana tu, mfano msaada wa masomo kwa wasichana.

- Swala moja lililolipuka miezi michache kabla hatujafika kisiwani mwezi Julai mwaka 2004 lilikuwa ni kuzoroteka kwa uhusiano baina ya kijiji cha Chole na hoteli. Hii ililetwa na ugumu wa kufanikisha mkataba wa kuwaunganisha, pia ilisababisha chuki kuelekezwa kwa CSWD kwa sababu ya kuwa Meneja Mradi ni mtunza hoteli.

- Kutokana na mgongano huu, meneja mradi alijiuzulu kutoka nafasi yake. Watathmini waliona kwamba ingesaidia kutofautisha majukumu ya mtunza hoteli na yale ya meneja mradi wa CSWD, walipendekeza kuteuliwa mara moja kwa Afisa Maendeleo ya Jamii kufanya kazi na CSWD.

- Chama cha wanawake cha Wanawake mbele/FOKUS kimekuwa si cha kawaida katika kutoa misaada mikubwa ya kifedha kwa vikundi vya umma katika jamii maskini sana. Kimefanya bidii kubwa sana kuwezesha kuwa na mawasiliano mazuri kati ya mfadhili na wapokeaji.

- Hata hivyo, malengo ya chama ya kuwapa uwezo kwa wanachama wa CSWD lazima yaonekane katika mazingira ambayo
  a) Umilikaji wa CSWD na rasilimali zake inabidi ujadiliwe na wenyeji
  b) Mambo yapewayo kipaumbele na CSWD si lazima yalingane na yale ya Wanawake mbele/FOKUS, ingawa mara nyingi yanalingana.

- Kutokana na sababu zilizotajwa hapo juu, watathmini waliona kuwa ni muhimu kwa CSWD kutilia mkazo mara moja uendelevu wa miradi kwa siku za karibuni badala ya kuanza miradi mipya.

Uendelevu wa kudumu wa miradi ni swala kubwa, na ambalo umuhimu wake unatambuliwa na viongozi na wahamasishaji wa CSWD pamoja na jamii yote kwa ujumla. Huu ni ugumu unaoibuka kutokana na kutegemea michango ya fedha za wafadhili (michango ambayo hutegemea hali zisizoweza kutabirika toka nje) katika jamii maskini yenye uwezo mdogo wa kuzalisha mfuko wao wenyewe wa fedha za kuendeleza miradi.



# 2

# Hitimisho na mapendekezo maalumu

## ‘Maendeleo’, ‘uendelevu’ na ‘uongezaji uwezo’

Neno “maendeleo” hutumika mara kwa mara huko Chole kama linavyotumika katika sehemu nyingine za Tanzania. Je, neno hili lina maana gani? Kwa watu wengi neno “maendeleo” linajumuisha uboreshaji wa hali ya maisha na nafasi katika maisha zinazoletwa kupitia upatikanaji mkubwa wa elimu, huduma za afya, na mafanikio ya kiuchumi. Maendeleo hutokea katika madaraja mawili, maendeleo ya jamii pamoja na yale ya mtu binafsi. Ingawa mara nyingi kuna makubaliano kuhusu ni matakwa yepi yanatamaniwa, maoni juu ya namna ya kuyapata huwa hayakubaliwi kwa pamoja.

CSWD, kama jumuia nyingine mbili zilizoko Chole (CSDS na CEDS), ni chama ambacho kinatakiwa kifanye shughuli za maendeleo. Hata hivyo, tofauti na jumuia hizi nyingine mbili kijijini, unachama wa CSWD na hasa faida zake una mipaka ya kijinsia. Miradi ambayo chama hiki inajishughulisha nayo kimsingi imeelekezwa kwa wanawake tu, ingawa mingi ya miradi hiyo hunufaisha wanaume pia. Walakini si kila mtu anakubali miradi ipi ipewe kipaumbele. Kwa mfano baadhi ya watu walionelea kuwa hali mbaya ya shule ya msingi na mgogoro wa kuchangisha fedha za Kituo cha Afya vilikuwa na umuhimu wa kugaramiwa zaidi kuliko masomo ya kompyuta.

Neno lingine linalotumika mara kwa mara sambamba na dhana ya maendeleo ni “uendelevu”. Wanakijiji wengi walilalamikia ukweli kwamba si miradi iliyopita tu bali hata miradi ya sasa mfano Kituo cha Afya, vimejenga uendelevu. Kwa ujumla fedha za kimataifa huelekezwa kwenye kuanzisha miradi na gharama za vifaa zaidi kuliko kwenye mishahara au gharama nyingine za kuendesha miradi hiyo ili wanakijiji waweze kuiendeleza. Mara nyingi inatarajiwa kuwa vijiji vitafute fedha za kuendeleza miradi, lakini hii si rahisi kwa kijiji kama Chole ambako uwezo wa kifedha unapungua badala ya kuongezeka hivyo inakuwa vigumu kuzalisha fedha kutegemea watu wa ndani ya kijiji. Wanakijiji hawana ujuzi wala mawasiliano na watu wanaoweza kuwa wahisani ili waweze kuandika miswada yao wenyewe kuchangisha fedha.

Neno la tatu linayotumiwa mara kwa mara na CSWD pamoja na shirika lake la wafadhili ni "uongezaji uwezo" au 'empowerment', dhana ambayo inaonekana kama lengo maalumu la chama hiki. Hata hivyo "uongezaji uwezo" si kitu pekee, bali ni tokeo la shughuli maalumu. Na je vipi kuhusu uongezaji- uwezo wa wanawake? Tumefurahi sana kuona maendeleo ya miradi ya CSWD na uwezo wa viongozi vyake. Walakini lazima tufahumu vizuri mazingira ya jamii ambamo rasilimali zinadidimia na wanaume wanahisi kuwa wana hali ngumu zaidi kulinganisha na vizazi vilivyopita pia kulinganisha na wanaume katika sehemu nyingine za Tanzania. Hivyo inakuwa vigumu kwa wanaume kukubali kwamba wanawake wanapendelewa zaidi yao. Sababu hii, matatizo ya sasa yanayokabiliwa na CSWD ndani ya jamii yanatokana na "ubaguzi wa kijinsia" uliopakazwa juu ya matatizo makubwa ya kimuundo.

Ukitilia maanani maswala haya, je CSWD itawezaje kustawi na kufanya kazi kwa amani na wanachama wake na wale wasio wanachama? Tunatoa mapendekezo katika vifungu vifuatavyo. Kwanza kabisa yabidi kutilia mkazo kuwa mengi ya mapendekezo haya yangeweza kutolewa na vyama vingine kijijini. Ni hakika kwamba tunaona inafaa kuwa kuna kiwango fulani cha utofauti katika njia za uongozi ambazo vyama hivi vitatu vinatumia kujiongoza. Wakati wa kutathmini tulitambua wazi kuwa CSWD ilikuwa chini ya uchunguzi mkali ambao vyama hivi vingine viliweza kukwepa.

## Uongozi

Kama ilivyotajwa hapo awali, tulisikia malalamiko juu ya uongozi wa CSWD ingawa lazima ifahamike kuwa mengi ya malalamiko haya yanahusu pia vyama hivi vingine vilivyoko Chole.

Tuliambiwa kuwa baadhi ya watu walikuwa wameshikilia ofisi za CSWD kwa muda mrefu sana, ingawa hii pia ni kweli kuhusiana na taasisi nyingine za kijiji zikiwemo Serikali ya Kijiji na vyama vingine viwili vilivyoko Chole. Ni muhimu sana kwa vyama kuleta watu wapya na mawazo mapya, lakini pia ni muhimu kuhakikisha mwendelezo, uimara na uwezo. Tunapendekeza kuwa vyama vyote vizingatie yafuatayo:

1. Kama itapendelewa kuwe na muda maalum wa kushika ofisi, ili kwamba baada ya mihula miwili ya kushika ofisi, watu wastaafu kuwezesha mtu mwingine kuchaguliwa.

2. Kama itapendelewa kuwe na uchaguzi wa kuzunguka ili kwamba kila mwaka kuwe na uchaguzi wa nusu ya viongozi wa ofisi na wanakamati wa kawaida. Kwa njia hii kutakuwa na mwendelezo wa uongozi na ujuzi.

3. Kama huko mbeleni viongozi watasafiri kwenda nje ya ya Mafia, ingefaa kutuma mchanganyiko wa wanachama wa zamani na wale wapya ili hawa wapya waweze kupata uzoefu wa namna ya kuwalikisha jamii yao.

Ilionekana kwamba baadhi ya viongozi wa CSWD walikuwa ndugu wa karibu, kwamba wengi wa wanakamati wa CSWD wanatoka katika vitongoji viwili vya kijiji na miradi yote ya majengo yaliwekwa katika sehemu hizo. Mapendekezo:

4. Kama kutakuwa na miradi mingine mipya au majengo mapya siku zijazo basi vijiji vya Kilimani na Mwapepo vizingatiwe kama sehemu za kuweka majengo na miradi hiyo.

5. Inabidi kuwe na angalau watu wawili kutoka katika kila kitongoji ya kijiji katika kamati ya kila chama na mtu moja katika kamati ndogo zake.

6. Kati ya washika ofisi wakuu (Mwenyekiti, Khatibu na Mweka hazina) walau watu wote wasitoke kitongoji kimoja tu cha kijiji. Utaratibu huu inapasa uanze kutumika kuanzia muda wa uchaguzi wa mwaka kesho.

7. Kwamba kuanzia uchaguzi ujao, watu watatu wenye jukumu la kuweka saini hund i (mbali ya PM na CDO) watoke katika vitongoji tofauti vya kijiji.

8. Baadhi ya mikutano ya kawaida ya CSWD ifanyike mahali pengine zaidi ya Mnyange, ingawa kamati labda itapenda kutumia ofisi yake.

## Meneja mradi/mshauri wa kiufundi wa CSWD

Kutokana na kukosa makubaliano baina ya hoteli na kijiji, tunafikiri itakuwa bora kama meneja mradi wa sasa asirudi tena kufanya kazi CSWD. Inaeleweka kuwa meneja huyu amefanya kazi kubwa sana kukisaidia chama na kwamba wanachama wanamshukuru sana kwa uongozi wake. Ni kweli kuwa wengi wa wanachama wa ndani wangependelea arudi kazini kwa muda wa kudumu, lakini kutokana na hali halisi iliyopo sasa baina ya hoteli na wanakijiji kuhusu makubaliano. Tunafikiri ingekuwa bora kama chama kingetafuta mwanamke mwingine kuwasaidia akina mama na miradi yao.

- Kazi ya Meneja Mradi mpya itakuwa kuandika ripoti, kuandika miswada, kuwavuta wanawake ambao hawajashirikishwa katika chama hiki, kuhimiza miradi yote iende mbele na kuweza kushirikisha vyama vingine kijijini, Serikali ya Kijiji, wilaya na Wanawake mbele/FOKUS. Zaidi ya hayo, aweze kufundisha watu namna ya kuendesha miradi yao ili wafanikiwe na pia kuandika ripoti zao wenyewe.

- Mshahara unaostahili mtu mwenye ujuzi kama huu sio mdogo kulingana na viwango vya kijiji, lakini ili kuhakikisha miradi ya CSWD iendelee mbele siku zijazo, itahitajika kuajiri mtu mwenye ujuzi wa kiwango hiki. Wakati wa kuandika ripoti hii, watathmini walikuwa tayari wameandika maelezo ya kazi hii na maelezo maalum ya mwajiriwa na walijadiliana haya na kamati ya CSWD. Pia wameanzisha kamati ya watu wanne ya kuorodhesha majina ya awali ya watakaohojiwa kwa kazi hiyo. Pia tumependekeza yafuatayo:

9. Meneja-Mradi wa sasa asirudi tena kwa muda mrefu kufanya kazi kwa CSWD.

10. Ateuliwe Meneja-Mradi mpya (Afisa Mendeleo ya Jamii) haraka iwezekanavyo.

11. Ateuliwe msaidizi wa Afisa Maendeleo (CDO) wakati Afisa mpya atakapokuwa madarakani na kuwa na muda wa kujadiliana na CSWD kuwa ni mtu wa aina gani atakayefaa.

## Kuendeleza mawasiliano, ushirikiano na uwazo

Tulisikia malalamiko kadhaa kuhusu mawasiliano, ushirikiano na uwazo. Malalamiko hayo yalitoka kwa wanawake ambao hawakujiona kama wao ni sehemu ya ndani ya wanachama hai wa CSWD, wengi wa wanakijiji ukijumuisha wanaume, na kutoka kwa baadhi ya wanakijiji walioko katika Serikali ya Kijiji.

Upelelezi wetu ulituonyesha kwamba CSWD ilijaribu sana kuwa na mawasiliano kadri ilivyoweza lakini si kila mara majaribio hayo yalifanikiwa. Sababu hii tunatambua kuwa mawasiliano na jamii kwa ujumla yanahitaji kuboreshwa katika viwango mbalimbali, yakiwemo yale ya kijiji na wilaya na nje zaidi. Lakini pia ni muhimu kwa jamii kwa ujumla kutambua kuwa maamuzi ya NGOs zote bidi yafanywe na wanachama wake kuliko wale wasio wanachama. Si vizuri kwa watu wengine kushiriki katika kupanga na ufanyaji maamuzi, hii ni kinyume na sheria zinazosimamia NGOs.

Wanakijiji wasio wanachama na wale wanachama wasio hai wanahisi kuwa wanahitaji kuelewa nini kinatokea na kwa nini, na pia wanataka kuelewa mgawanyo wa rasilimali; kwa hiyo tunapendekeza kwamba CSWD (na vyama viwili vilivyopo) vizingatie yafuatayo:

12. Nakala ya jadala la kila chama iwekwe katika Kituo cha Kujifunza kwa ajili ya matumizi ya umma.

13. Maelezo ya CSWD na vyama vingine vilivyoko kijijini yatolewe kila mara na kupewa vijana wa Kituo cha Kujifunza kwaajili ya kuchapishwa kwenye makala mpya ya gazeti dogo la chama.

14. Vibao visimamishwe katika kila sehemu ndogo ya kijiji kutoa taarifa kuhusiana na shughuli zinazotokea.

15. CSWD inafikiria kutumia mjumbe wa kulipwa ambaye atakuwa akitoa taarifa muhimu za haraka kwa njia ya baiskeli.

## SERIKALI YA KIJIJI

Tuliambiwa kuwa ingawa Serikali ya Kijiji ilitoa rukhusa ya miradi mikubwa (mfano ujenzi wa Chekechea au Kituo cha Mafunzo) na kuwa ilikuwa ikipata nakala za bajeti mara kwa mara, mara nyingi haikuulizwa mawazo yake kuhusiana na mipango ya baadaye ya CSWD.

Hata hivyo, wakati wa ziara yetu na CSWD ilionekana kwamba tayari ilisha anza kujaribu kushirikiana zaidi na Serikali ya Kijijina ikitegemea kuendelea utaratibu huo. Ni muhimu sana kwa Serikali ya Kijiji kupata taarifa za miradi na mambo yafanyikayo katika chama hiki (na hasa pia yale ya vyama vingine vyote) wakati huo huo CSWD itabaki huru na yenye kujitawala kama NGO. Pia ni muhimu kuwe na ushirikiano mkubwa na kubadilishana mawazo na ripoti za maendeleo kati ya vyama hivi vitatu na Serikali ya Kijiji. Kwahiyo tunapendekeza yafuatayo:

16. CSWD ishauriane na Serikali ya Kijiji kabla ya kukamilishamipango yake kwa mwaka unaofuata ingawa uamuzi unabaki na CSWD.

17. CSWD ihakikishe kuna nakala za Kiswahili za maazimio yake yote, ripoti, bajeti na mahesabu zitakazopelekwa katika Serikali ya Kijiji, ambayo itoe risiti. Nakala ya kila ripoti iwekwe katika Kituo cha Mafunzo.

18. Kutakapokuwa na uchaguzi wa chama chochote kile, mwenyekiti wa kijiji na mjumbe mmoja (au zaidi) wa baraza wawepo kama mashahidi. Mashahidi haya wapeleke ripoti kuihusu uchaguzi ka VC.

19. Mikutano ya mihula ya mwaka ya vyama hivi vitatu pamoja na Serikali ya Kijiji iliyokuwa ikifanyika ianzishwe tena.

20. Mkutano wa mwaka wa usimamizi wa wanachama wote wa CSWD uwaalike wawakilishi kutoka Serikali ya Kijiji na kutoka katika vyama vingine kama waangalizi. Vyam vingine vile vile waanze mikutano ya mwaka wa usimamizi.

21. Wanakijiji wengine yapasa waelewe kuwa kila chama kina haki ya kujitawala na taratibu za kufanya maamuzi yake yenyewe.

22. Ni vizuri wanachama wakutane mwanzoni mwa mwaka ili wapange mipango ya mwaka unaofuata. Baada ya kufanya hivyo wakutane na Serikali ya Kijiji kupata mawazo yao juu ya mipangoyao ya siku za usoni. Hii inaonyeshwa katika ratiba ifuatayo ya CSWD:

**Mpango wa ratiba ya mwaka**

| | |
|---|---|
| Machi | CSWD kujadili mipango ya mwaka ufuatao. |
| Aprili | Kamati ya CSWD kuwasiliana na baraza la Kijiji (VC) pamoja na kamati ya vyama vingine kuhusu mipango hiyo. |
| Juni | CSWD kuandika ripoti ya nusu mwaka, nakala ya Kiingereza kwa FOKUS, nakala ya Kiswahili kwa Serikali ya Kijiji<br>Kumalizia maazimio ya mwaka unaofuata. |
| Julai | Kutuma maazimio kwa FOKUS |
| Septemba | Jibu kutoka kwa FOKUS. Nakala ya majibu kutumwa kwa Serikali ya Kijiji |
| Novemba | Kumaliza mahesabu ya bajeti.<br>Kujadili nini cha kufanya na fedha zozote zilizobakia, na kushiri kiana na baraza la kijiji na vyama vingine kuhusiana na hili.<br>Kuomba ruhusa toka kwa Wanawake mbele/FOKUS kutumia hela inazobaki kwa ajili ya Kituo cha Afya |
| Desemba | Kutuma kwa mhasibu. Kuandika ripoti ya mwaka na kuituma Norway.<br>Nakala ya Kiswahili ipelekwe katika baraza la kijiji (VC). |

Ni muhimu pia kuwa na mawasiliano kamilifu na utawala wa wilaya. Maelezo juu ya CSWD tayari yanapatikana katika ofisi za Mkuu wa Wilaya (DC), pia

katika idara mbali mbali za Makao Makuu ya Wilaya, ikiwemo idara ya Elimu, Maendeleo ya Jamii na Vyama vya Ushirika. Tuna pendekeza yafuatayo:

23. Nakala za ripoti za mwaka na mahesabu yalikaguliwa zitumwe kwenye ofisi za DC, DED (Mkurugenzi) na DAS (Khatibu Mtengaji ya Wilaya), na nakala za nyaraka nyingine zitumwe kwaidara zinazohusika, ikiwemo ofisi ya Khatibu Tarafa ya Kusini. Risiti zipatikane.

CSWD ni chama ambacho kimesajiliwa katika Msajili Mkuu wa Vyama vya Tanzania na inalipa mchango wake kwa Msajili kama inavyotakiwa.
Mapendekezo:

24. Nakala za katiba, cheti cha usajili na nyaraka nyingine muhimu ziwasilishwe katika Kituo cha Mafunzo.

### MAWASILIANO NA MFADHILI

Lugha kuu ya mawasiliano na mfadhili wa Norway ni Kiingereza, lugha ambayo hakuna mwanachama yeyote wa kamati ya CSWD anaweza kuongea au kuandika katika kiwango chochote kile. Hata hivyo mfadhili anaweza kupata nyaraka za tafsiri za Kiswahili zinazotumwa na CSWD. Walakini, kutumia posta kama njia ya mawasiliano ni taratibu mno na inaleta usumbufu mwingi, ingefaa zaidi kutumia barua pepe (email). Kwahiyo basi tunapendekeza yafuatayo;

25. Washika ofisi wawili wa CSWD ambao tayari wameshajua kutumia compyuta kidogo, wafundishwe namna ya kutumia barua pepe (‘email’) pamoja na namna ya kuambatanisha nyaraka (attachment), na kuanzisha akaunti ya hotmail au yahoo ili waweze kutumia “internet cafe” iliyoko Utende kwa mawasiliano na mfadhili. Baada ya uchaguzi ujao, washika ofisi wengine nao watapata mafunzo kama wenzao.

## Mgawanyo wa faida, mgawanyo wa majukumu

### KUNUFAISHA WANAWAKE WOTE

Watu wengi walitulalamikia kuwa CSWD haishirikiani vizuri na watu wa nje, hapa wanagusia baadhi ya wanawake (hasa wale wanaoishi katika kitongoji cha Kilimani) ambao hawahudhurii mikutano au hawashiriki katika shughuli za CSWD. Walakini, kama wanawake hawa wanaona wameachwa nje na wanataka kufaidika na CSWD, ni lazima wahudhurie mikutano, wajitayarishe kufanyia kazi

za chama, na kupiga kura kwa viongozi wao. Kwa sasa, wanawake wote wanaoishi Chole ambao wanaumri zaidi ya miaka 18 ni wanachama pende wasipende. Tunapendekeza yafuatayo:

26. Kwamba CSWD ifikirie kuainisha uanachama ili ueleweke zaidi, kwamba wanawake wajaze fomu za kujiandikisha na wakubali kushiriki katika miradi mbali mbali ya CSWD.

27. Bidii kubwa ifanywe kuwavuta wanawake wanaoishi kitongoji cha Kilimani.

28. Wanawake wote wa Chole watambue kwamba wakitaka sauti zao zisikiwe na wakitaka kufaidi na CSWD, inafaa kuhudhuria katika mikutano na kuingia katika miradi ya CSWD.

### KUNUFAISHA JAMII UJUMLA

Kulikuwa na malalamiko mengi kwamba CSWD haikugawa faida zake kwa wanaume wa kijiji. Hata hivyo, ni muhimu ieleweke kuwa nia ya mfadhili wa CSWD Wanawake mbele/FOKUS, ni kusaidia wanawake wengine. Haya ni madhumuni na malengo yake – sio kwamba viongozi wa CSWD hawataki kuwasaidia wanaume. Ukweli ni kwamba wengi wa wanachama wa CSWD wenyewe walisema kuwawangependa kuwa na uwezo wa kuwasaidia wanaume, hasa watoto wao wa kiume. Hata hivyo, CSWD lazima ifuate bajeti ambayo imekubaliwa na mfadhili wa chama na haina uhuru wa kubadilisha mipango yake kipekee. Kwa upande mwingine, ingawa miradi mingi ni kwa ajili hasa ya wanawake (kama vile soko, mipango ya Akiba na Mikopo na msaada wa ada kwa watoto wa kike kwenda sekondari) Miradi mingine hunufaisha wanaume na wanawake vile vile (Mfano: Chekechea, Kituo cha Kujifunzia, madarasa ya elimu ya watu wazima pia programu ya utambuzi wa UKIMWI). Isitoshe, desturi imekuwa kuomba mfadhili aruhusu mabaki ya fedha zozote mwishoni mwa mwaka zipatiwe zahanati kununulia dawa, huduma nyingine ambayo inawanufaisha wakazi wote wa Chole.

29. Tunapendekeza kuwa wanawake wa CSWD waamue wenyewe jinsi wanvyotaka utumia msaada huo, kwa mfano wakitaka kuwapa baadhi ya wanafunzi wa kiume msaada wa ada za shule ya sekondari.

## Namna ya kukabili magomvi katika jamii

Ni muhimu sana kwa watu wa Chole kuwa na njia ya kuamua magomvi kabla hayajawa matatizo makubwa ambayo yatazuia miradi ya vyama vya Kijiji. Tuna mapendekezo yafuatayo ambayo yanaweza kusaidia.

30. Kama mtu anafikiri kuwa mtu mwingine kutoka chama chochote kile anafanya vitu ambavyo hatakiwi kufanya, mtu huyo achague mwenzake na kwenda kwa Mwenyekiti wa Kijiji aidha kwa usuluhishi au kupeleka malalamishi. Mwenyekiti wa kijiji anaweza kumwita mwenyekiti wa chama kinachohusika au mtu mwingine yeyote, ili kuangalia ukweli na kuamua ugomvi. Anaweza kufanya hivi kwa siri au kiofisi kutegemea pande zote mbili zitakavyoona inafaa.

31. Lakini kama mtu anamtuhumu mwingine bila ushahidi, aletwe mbele ya Serikali ya Kijiji kwa madai ya kuharibu mahusiano katika jamii.

## Kipindi cha kati na kirefu cha hali ya baadaye ya CSWD

CSWD kwa sasa iko katikakati ya awamu ya miaka mitatu ya fedha, kuanzia mwaka 2003 na kuishia mwishoni mwa 2005. Miswada imeshakusanywa kwa ajili ya kupatiwa fedha kwa mwaka ujao, 2005. Inaelekea kuwa CSWD imefanya maamuzi kadhaa kwa uzingatifu:

- Kuimarisha miradi iliyoko sasa badala ya kuanzisha mingine mipya.

- Kuhairisha kuzifikia jamii jirani badala yake kunuia kuwavuta wanawake wa Chole ambao mpaka sasa hawajashiriki katika kiwango chochote kile katika CSWD.

- Kuboresha matarajio ya kielimu ya watoto wa Chole kwa kuwapa ‘tuition’ (yaani madarasa zaidi) ambayo itawawezesha wengi wao kwenda sekondari.

- Kujibu hitaji lililotajwa katika kila mkutano tuliohudhuria la kutenga wadi ya uzazi katika Kituo cha Afya.

Tungekubali miswada hii yote na kufadhili mgawanyo wa fedha katika miradi hii. Zaidi ya hayo tunapendekeza kwamba CSWD na Wanawake mbele/FOKUS

wafikirie namna gani miradi ya sasa inaweza kufanywa ya kudumu, hasa kama mhisani maalum hataendelea kutoa msaada baada ya 2005.

32. Tungependa kupendekeza kuwa mfadhili afikirie kuendeleza mchango kwa gharama zinazojirudia za miradi iliyopo, kama vile Kituo cha Afya cha Chole, chekechea na Kituo cha Mafunzo.

33. Ukizingatia umuhimu hususan wa Kituo cha Afya cha Chole, pamoja na hali yake mbaya ya kifedha na kushindwa kwetu kutoa tathmini hakiki ya namna kituo hiki kinavyoendeshwa, tunapendekeza kuwa Dr Rob Barbour aalikwe kuja kukagua kwa makini ubora wa kituo hiki siku za karibuni. Ukaguzi huu utawapa nafasi wafanyakazi wa zahanati kueleza mambo yanayoihusu zahanati kwa mtu mwenye ujuzi wa kidaktari na mwenye historia ndefu na Chole, wakati huo huo kusaidia kutoa mawazo ya kimsingi ya jitihada za mbeleni za kupata wafadhili kutoka nje.

Ikiwa kama awamu mpya ya mfuko wa fedha utaanza baada ya 2005, tunafikiri kwamba hii itegemee vipengele vifuatavyo:

- Mafanikio ya uteuzi wa Afisa Maendeleo wa Jamii au Community Development Officer (CDO) ambaye atasaidia kuendeleza miswada mipya na kuhakikisha inafanikiwa.

- Kuonyesha kwa uhakika kuwa CSWD inaishirikisha wanawake wote wa Chole.

34. Na kwa uhakiki huo huo, tunapendekeza kuwa shughuli zote za CSWD ikiwa ni pamoja na mikutano iweke sehemu ya usimamizi ambayo itatoa maelezo juu ya wakazi washiriki au wafaidikaji kutoka sehemu ndogo ndogo za kijiji.

Pat Caplan 071104, 211104